EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# TAARIFA KWA UMMA

## MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP LTD), WATANGAZA KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA YA UFADHILI.

Kampala, Uganda : Tarehe 26 Machi, 2025

EACOP Ltd., ni kampuni inayosimamia ujenzi na hatimaye uendeshaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka eneo la Kabaale nchini Uganda hadi Tanga nchini Tanzania. Kampuni hii inayo furaha kutangaza kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ufadhili wa fedha za nje zilizotolewa na muungano wa taasisi za fedha pamoja na benki za kikanda kama vile African Export Import Bank (Afreximbank), The Standard Bank of South Africa Limited, Stanbic Bank Uganda Limited, KCB Bank Uganda na Islamic Corporation for the Development of the Private Sector (ICD).

Kukamilika kwa awamu hii ya kwanza ya ufadhili wa fedha za nje ni kiashiria cha mafanikio makubwa kwa EACOP LTD na wabia wake ambao ni TotalEnergies (TTE 62%), Uganda National Oil Company Limited (UNOC 15%), Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC 15%) na CNOOC (8%). Hatua hii inadhihirisha uungwaji mkono wa mradi huu na taasisi za fedha katika kuleta mabadiliko makubwa ya miundombinu kikanda.

Nchini Uganda na Tanzania, ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki unaendelea vizuri na kuweka kipaumbele katika masuala ya usalama, uboreshaji wa mazingira, pamoja na ushirikishwaji wa jamii.

Kwa ujumla, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2024, maendeleo ya mradi yalifikia na kuzidi asilimia hamsini (50%). Hadi sasa, zaidi ya wananchi elfu nane (8,000) kwenye nchi za Uganda na Tanzania wameajiriwa na takriban masaa laki nne (400,000) ya mafunzo yametolewa na kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni Mia Tano ($500M) zimetumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma katika nchi hizo.

Miundombinu ya mfumo wa kimataifa ya usafirishaji wa mafuta.

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ni miundombinu ya usafirishaji wa mafuta ghafi kutoka eneo la Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda hadi eneo la Chongoleani Peninsula katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kuuzwa katika masoko ya kimataifa. Mfumo huu unajumuisha mabomba yaliyofunikwa (insulated) yenye kipenyo cha inchi 24, vituo sita (6) vya kusukuma mafuta, vituo viwili (2) vya kupunguza kasi ya mafuta, na kituo cha usafirishaji mafuta ghafi cha baharini chenye mfumo wa jua wa megawati tatu (3MWp) kilichounganishwa na gridi ya taifa kwa ajili ya usambazaji umeme. Mradi huu umejikita katika utekelezwaji wenye viwango vya juu vya kimataifa vya mazingira na jamii kama vile vya Shirika la Fedha la Kimataifa (International Finance Corporation IFC) na Kanuni za Ikweta (Equator Principles)

Baada ya kukamilika kwa ujenzi, bomba hili litakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa ya mafuta ghafi laki mbili na elfu arobaini na sita (246,000) kwa siku. Mfumo huu mkubwa wa usafirishaji una urefu wa kilomita elfu moja mia nne na arobaini na tatu (1,443). Aidha, urefu wa kilomita mia mbili tisini na sita (296) zipo Uganda na kilomita elfu moja mia moja na arobaini na saba (1,147) zipo nchini Tanzania.

www.eacop.com

For more information, contact: **info@eacop.com | TZ +255 699 022 905 | UG +256 767 988 008**